

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

**MWITO WA KUPATA MAONI YA WADAU KUHUSU MAREKEBISHO YA
KANUNI ZA UWEKAJI NA USAMBAZAJI MIFUMO YA UMEME, 2019.**

Kwa mujibu wa kifungu Na 8 (3) na 45 cha Sheria ya Umeme Na 131, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ina mamlaka kisheria ya kutengeneza kanuni za kusimamia shughuli za ufungaji umeme kwa wenye leseni nchini.

Mwaka 2015, EWURA ilitengeneza Kanuni za Uwekaji na Ufungaji Umeme, ambazo zilianza kutumika rasmi tarehe 11 Septemba 2015, baada ya Kupitishwa na Wizara husika na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 404. Hata hivyo, tangu kuanza kutumika kwa kanuni hizo, zimejitokeza changamoto mbalimbali.

Moja ya changamoto hizo, ni kubadilika kwa mitaala katika vyuo vya ufundi-VETA nchini na vyuo vingine vinavyotoa mafunzo ya uwekaji na usambazaji umeme na kupelekea EWURA kutoa madaraja ya leseni yasiyoendana na mabadiliko ya hayo kwa kuendelea kutumia Kanuni za mwaka 2015.

EWURA imepitia upya Mtaala wa masomo wa vyuo vya VETA, Vyuo vikuu, na Taasisi nyingine zinazotoa elimu ya masuala ya umeme ili kukidhi mabadiko hayo katika kanuni.

Kwa mantiki hiyo, EWURA imeandaa mkutano wa taftishi ili kukusanya maoni kutoka kwa wadau utakaofanyika tarehe **12 Februari 2019** katika Ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki zilizopo Jengo la LAPF, Mkabala na kijiji cha makumbusho, gorofa ya saba, kuanzia **saa nne kamili asubuhi**.

Wadau wanaopenda kutoa maoni yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kumwandikia Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonyeshwa hapo juu kabla ya **4 Februari 2019** au kupitia barua pepe info@ewura.go.tz. Rasimu ya kanuni mpya za mwaka 2019 inapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.ewura.go.tz, Ofisi ya Makao Makuu na Ofisi zote za Kanda wakati wa muda wa kazi kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni. Wadau wanaombwa kuzingatia muda uliopangwa wa kutoa maoni yao ili kufanikisha zoezi hili. Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kumwandikia Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoatajwa hapo juu.

**Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**